**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 19 Aprili, 2016**

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunawakaribisha tena katika Mkutano wetu wa Tatu, Kikao cha Kwanza, Katibu.

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliapa:

1. Mhe. Lucy Fidelis Owenya

2. Mhe. Oliver Daniel  Semuguruka

3. Mhe. Ritta Enespher Kabati

4. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tuendelee baada ya mechi hii ya asubuhi ya magoli matatu kwa moja, Katibu! *(Makofi/Kicheko)*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu tarehe 15 Januari, 2016 kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 3 la Tarehe 15 Januari, 2016;
(ii) Toleo Na. 4 la Tarehe 22 Januari, 2016;
(iii) Toleo Na. 5 la Tarehe 29 Januari, 2016;

(iv) Toleo Na. 6 la Tarehe 05 Februari, 2016;
(v) Toleo Na. 7 la Tarehe 12 Februari, 2016;
(vi) Toleo Na. 8 la Tarehe 19 Februari, 2016;
(vii) Toleo Na. 9 la Tarehe 26 Februari, 2016;
(viii) Toleo Na. 10 la Tarehe 4 Machi, 2016;
(ix) Toleo Na. 11 la Tarehe 11 Machi, 2016;
(x) Toleo Na. 12 la Tarehe 18 Machi 2016;
(xi) Toleo Na. 13 la Tarehe 25 Machi, 2016;
(xii) Toleo Na. 14 la Tarehe 01 Aprili, 2016; na
(xiii) Toleo Na. 15 la Tarehe 08 Aprili, 2016.

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri tunakushukuru sana. Katibu!

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyo ada. Swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu.

Na. 1

**Uchaguzi kwenye Kata ambazo uchaguzi haukufanyika**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Katika Jimbo la Ulyankulu, Kata za Milambo, Igombemkulu na Kamindo bado hazijafanya uchaguzi:-

Je, ni lini Kata hizo zitafanya uchaguzi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU (MHE. DKT. ABDALLAH S. POSSI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupitia Tangazo la Serikali Na. 295 la Tarehe 23 Julai, 2015 ilitangaza jumla ya Kata 3,946 kwamba ndizo zitakazoshiriki uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara katika uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba, 2015. Kata za Kamindo, Igombemkulu na Milambo hazikujumuishwa katika orodha hiyo kwa kuwa ni maeneo mapya yaliyowasilishwa na Serikali baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwa imekamilisha maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2015.

Vilevile zoezi la utoaji uraia (*naturalization*) na utangamanisho (*intergration*) kwa baadhi ya wakimbizi bado linaendelea katika maeneo hayo. Zoezi hilo litakapokamilika taratibu za kisheria zilizopo zitazingatiwa kabla ya kufanya uchaguzi katika maeneo husika.

**MHE. JOHN P. KADUTU**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninamuomba awahakikishie wananchi wa Kata hizo kwa sababu siyo wote ni wakimbizi, ni lini zoezi hilo la *naturalization* litakamilika ili kusudi nao wapate kutimiza haki yao ya kidemokrasia? *(Makofi)*

**SPIKA**: Majibu ya swali hilo Mheshimwa Naibu Waziri Possi ni lini, Mheshimiwa Selemani Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, mchakato pale ulikuwa ni mpana sana, kama alivyosema pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba zoezi lile lilikamilika na kuhakikisha Kata zinapatikana lakini ilikuwa ni baada ya uchaguzi, baada ya hapo kuna zoezi kubwa la *integration* ambalo linafanyika ambalo lina-*involve* pesa na awali mchakato uliokuwa unaendelea ni suala zima la kupata fedha kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu Serikali ime-*invest* vya kutosha kuhakikisha wakimbizi hawa wanakuwepo maeneo haya kipindi chote, maana yake Serikali ya Tanzania ilitumia jukumu kubwa la kiutu na kiubinadamu na *resources* nyingi sana kuhakikisha wakimbizi hawa wanakuwepo, lakini suala la kuhakikisha unajenga miundombinu ni jambo lina-*involve* pesa.

Kwa hiyo, Serikali iko katika mchakato kuangalia jinsi gani tutafanya, suala la kujenga *structure* zikamilike baadaye basi uchaguzi uweze kufanyika, kwamba sasa eneo lile uchaguzi ufanyike rasmi baada ya kuwa na muundo rasmi wa Serikali za Mitaa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, kwa niaba yake tafadhali endelea.

Na. 2

**Zahanati ya Kitunda kufanywa Kituo cha Afya**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA)** aliuliza:-

Zahanati ya Kitunda inahudumia wananchi wa Kata za Kitunda, Kivule, Kipunguni, Msongola na baadhi ya wananchi toka Chamazi na Tambani katika Mkoa wa Pwani.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuifanya zahanati hiyo kuwa Kituo cha Afya ili kiweze kumudu mahitaji makubwa ya wananchi wa maeneo yaliyotajwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Kitunda iliyopo Kata ya Kitunda haina eneo la kutosha kukidhi ongezeko la miundombinu inayohitajika kuwa kituo cha afya jambo ambalo litalazimu Serikali kuwaondoa wananchi na kulipa fidia. Ili kuboresha huduma za afya katika Kata ya Kitunda, Kivule, Kipunguni na Msongola na maeneo jirani, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imeanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya katika Kata ya Kivule.

Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 zimetengwa shilingi milioni 900 na tayari ujenzi uko katika hatua ya msingi. Vilevile katika bajeti ya mwaka 2016/2017 zimetengwa shilingi bilioni moja ili kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa hospitali, Serikali imepanga kujenga zahanati mpya na kuimarisha zilizopo. Kutokana na juhudi za kufanikisha jambo hilo muhimu Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 600 katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya

ujenzi wa zahanati ya Lubakaya, Mbondole na Luhanga pamoja na nyumba za watumishi zilizopo katika Kata ya Msongola.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa jumla ya shilingi milioni 659.13 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na nyumba za watumishi katika Kata mpya ya Mzinga na Kipunguni B katika Kata ya Kipunguni.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua hii Hospitali ya Wilaya ambayo inajengwa hapo Kivule inagharimu kiasi gani kwa sababu mpaka sasa hivi anasema zimeshatoka shilingi milioni 1.9?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mkoa wa Dar es Salaam kwa ujumla una idadi kubwa sana ya wananchi na hospitali nyingi zimepandishwa hadhi. Kwa mfano, Hospitali ya Amana - Ilala ambapo wananchi wa Kivule wanakwenda pale, lakini mpaka leo huduma za afya bado ni mbovu sana.

Je, sasa Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba hospitali hizi zinazopandishwa hadhi ikiwemo na hii inayojengwa, inakidhi mahitaji ili wananchi waweze kupata huduma ya afya ambayo ni haki yao ya msingi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kama alivyosema ni kweli sehemu ya Kivule ina changamoto kubwa sana, ndiyo maana tumeamua ujenzi wa ile hospitali ya Wilaya na kwa miundombinu yote mpaka inakamilika, hospitali ya Wilaya inagharimu takriban bilioni 24, lakini katika zoezi la kwanza ambapo katika bajeti niliyosema kwamba kumetengwa shilingi milioni 900 ya kwanza, na mkandarasai yuko *site* na ameshaanza *stage* ya *foundation.* Mkataba uliosainiwa na *Skol Building Contractors Limited* utagharimu karibu shilingi bilioni moja na milioni 19.

Mheshimiwa Spika, huu ujenzi maana yake utafanikisha sasa angalau sehemu ya *OPD* ianze kukamilika, katika sehemu ya pili ni kwamba Hospitali ya Amana imepandishwa hadhi ni kweli, lakini ukiangalia Manispaa ya Ilala ni eneo lina changamoto kubwa sana na ndiyo maana tunajenga Hospitali ya Kivule. Sambamba na hilo kwa sababu Jimbo la Ilala ni pana, kulikuwa na harakati ya kujenga sehemu maalum ya akina mama na watoto katika eneo la Chanika katika kituo cha afya cha Chanika.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla kwamba ni nini kimefanya katika maeneo hayo ni kupandisha vituo viwili vya Pugu pamoja na Chanika, sambamba na hilo maana yake jambo linalofanyika maeneo ya kati ya Ilala ambayo imetanuka kuna zahanati nyingi ambazo nimezisema pale awali ambazo zinafanyiwa ukarabati na zingingine kuhakikisha kwamba vituo vyake vya afya vinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa hii hospitali ikipandishwa hadhi itaweza kufanyakazi vizuri, ndiyo maana katika bajeti ya mchakato wa mwaka huu mtaona kwamba bajeti ya Wizara ya Afya itakuwa imejielekeza kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba bajeti ya dawa

inaongezeka kwa kiwango kikubwa kukidhi hili ongezeko la watu na ongezeko la mahitaji ya wananchi katika sekta ya afya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, swali linaulizwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 3

**Viongozi wa Kitaifa Kutembelea Zanzibar**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

(a) Je, ni viongozi wangapi wa Kitaifa wametembelea Zanzibar kuanzia mwaka 2010 - 2015?

(b) Je, Serikali haioni kwamba viongozi wa Kitaifa kutembelea Zanzibar inaleta chachu ya upendo kwa Wananchi na kuzidi kuimarisha Muungano wetu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi 2015, viongozi wote wa Kitaifa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walitembelea Zanzibar.

Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitembelea Zanzibar mara 20, Mheshimiwa Dkt. Gharib Mohammed Bilal ametembelea Zanzibar zaidi ya mara 30 na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, ametembelea Zanzibar zaidi ya mara 12.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na hoja kuwa, Viongozi wa Kitaifa kutembelea Zanzibar inaleta chachu ya upendo kwa wananchi na kuzidi kuimarisha Muungano wetu. Ziara za viongozi wa Kiataifa huambatana na kuangalia utekelezaji wa shughuli za kijamii, kiuchumi na kisiasa, kuongea na wananchi na kutoa maagizo na maelekezo kwa viongozi wa Serikali. Aidha, ziara hizo zinatoa fursa ya kufanya mazungumzo na viongozi wa kisiasa wa Zanzibar hali ambayo pia inastawisha Muungano wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia swali la nyongeza

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Waziri amelijibu vizuri swali hili na vilevile linatoa siha kwa Watanzania, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mawaziri Wadogo katika miaka 1964 mpaka 1970 *station* yao ya kazi ilikuwa Zanzibar ili wapate kuelewa, Mawaziri wanabakia Bara, Mawaziri Wadogo ambao walikuwa na Wizara zao za Muungano huwa wanabakia Zanzibar. Je, Mheshimiwa Waziri suala hili analionaje kwa upande wa Wizara za Muungano?

(b) Kwa kuwa Mawaziri wa Muungano wana haki kuwepo Zanzibar mara kwa mara kutembelea katika taasisi zao za kazi, kwa nini wasijipangie kila baada ya miezi mitatu wabakie Zanzibar angalau kwa wiki moja kuona maendeleo ya Zanzibar na kuweza kupata ukweli wa utendaji wa kazi uliokuwepo pale? Asante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu Mawaziri Wadogo hasa wenye zile Wizara ambazo zinahusu Muungano kubaki Zanzibar, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi ni Mawaziri ambao ni wasaidizi wa Mawaziri wetu ambao tuko katika hizi Wizara za Muungano, ninachotaka nimhakikishie tu ni kwamba siyo tu kubaki Zanzibar, tutafanya kazi ya kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri katika maeneo yote yanayohusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kumhakikishia kwa dhati kabisa ni kwamba Mawaziri hawa na mimi mwenyewe nikiwepo, na ofisi yangu ambayo iko Ofisi ya Makamu wa Rais pale Tunguu Zanzibar, nimepanga ratiba ya kuwepo ofisini pale mara kwa mara, shida zote na majukumu yote yanayonihusu mimi kwa maana ya wananchi wa Zanzibar watanipata kwa urahisi sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa sababu ofisi hii ndiyo ambayo inaratibu mambo ya Muungano, Wizara zote zinazohusu Muungano tumeshatoa maelekezo ya Mawaziri na Naibu Mawaziri kuhakikisha kwamba katika maeneo yao wanatenga muda mwingi wa kuwepo Zanzibar ili wananchi wa Zanzibar wasipate shida ya kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, hivyo ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Naibu Mawaziri hatutapungua Zanzibar na wala hatutapungua upande mwingine, tupo mahali popote kwa ajili ya kushughulikia matatizo yote ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Waziri wangu wa Muungano kuwepo kule mara kwa mara ni hivyo hivyo kwamba tumeshakubaliana ofisini mimi na Waziri wangu na mpaka sasa hivi anaenda mara kwa mara tu Zanzibar. Mheshimiwa Mbunge ametutaka *at least* kwa miezi mitatu tuwe kule, lakini sisi karibu kila mwezi tunaenda Zanzibar na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar hawaoni *gap* lolote linalohusu mambo ya Muungano. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea. Bado tuko Wizara hiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Edward Franz Malongo,, Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 4

**Uchafuzi wa Mazingira Nchini**

**MHE. JORAM I. HONGOLI (K.n.y. MHE. EDWARD F. MWALONGO)** aliuliza:-

Uchafuzi wa Mazingira unaosababishwa na mifuko ya plastiki ni mkubwa mno nchini:-

(a) Je, Serikali haioni sasa umefikia wakati wa kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwawezesha wadau wa mazingira kwa kuwanunulia mashine kwa mkopo ili waweze kuchakata plastiki hizo kuzifanya kuwa ngumu na bora zaidi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili, bado tupo Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Luhaga Joelson Mpina

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu wa kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki nchini. Katika kutekeleza hatua hii Serikali imepitia upya kanuni ya kuzuia uzalishaji, uagizaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki ya mwaka 2006 ambayo ilikuwa inapiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki iliyo chini ya makroni 30 ambazo zilionekana kuwa na changamoto katika utekelezaji wake. Hivyo Serikali iliandaa Kanuni mpya ya matumizi ya mifuko ya plastiki ya mwaka 2015. Kanuni hizi zinaifuta kanuni ya mwaka 2006 na kuweka viwango vipya vya mifuko na vifungashio vya plastiki kuwa na unene usiopungua makroni 50 ambayo ina uwezo wa kuoza kirahisi kwenye mazingira ukilinganisha na ile ya makroni 30.

Pamoja na kuongeza unene wa mifuko ya plastiki, kanuni hii inapiga marufuku uanzishwaji wa viwanda vipya vya kutengeneza mifuko, vifungashio vya plastiki na pia inapiga marufuku uingizaji nchini wa mifuko ya plastiki ambayo ipo chini ya kiwango vilivyobainishwa na Kanuni. Hatua hii ni mwanzo wa kuelekea katika lengo la kupiga marufuku kabisa *(total burn)* uzalishaji na matumizi ya mifuko na vifungashio vya plastiki nchini kwa kuzingatia maoni ya wadau.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwekezaji katika sekta ya mazingira na kuhamasisha uwekezaji katika teknolojia rafiki wa mazingira, Serikali inaandaa kanuni na taratibu za nyenzo za kiuchumi zitakazotoa ruzuku, makato na punguzo la kodi kwa wawekezaji ili kuendeleza na kuimarisha utunzaji wa mazingira. Hatua hii itasaidia wadau wa mazingira kuwekeza katika viwanda vidogo na vikubwa vya uchakataji wa taka ikiwemo taka za plastiki.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Je ni lini sasa Serikali itaanza kutoa elimu kwa wananchi juu ya madhara yanayotokana na hii mifuko ya plastiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, tunaanza leo kutoa elimu ya uzingatiaji wa matumizi ya mifuko ya plastiki, wananchi waweze kuzingatia hilo, Sheria na kanuni hii yetu ya 2015 kwamba matumizi ya plastiki ambayo yanayoruhusiwa ni yale tu yenye makroni 50. Kwa hiyo, ni jukumu la Bunge hili na Wabunge wote, wadau wote na wazalishaji na wenye viwanda kuchukua jukumu na kuhakikisha kwamba plastiki zinazozalishwa ni zile tu zenye makroni 50 ambazo ndizo zimeruhusiwa na Kanuni, zaidi ya hapo hairusiwi na haikubaliki na watu watakaoenda kinyume watachukuliwa hatua kali za kisheria, tutachukua hatua kali kwenye viwanda ambavyo vitazalisha zaidi ya kiwango hiki kilichoruhusiwa ikiwa ni pamoja na kufunga kabisa viwanda hivyo. Hatutaruhusu matumizi hayo kwa namna yoyote yatumike nchini. Kwa hiyo, ni jukumu la Bunge hili, ni jukumu la wananchi wote, kuelewa kwamba plastiki iliyoruhusiwa ni ile yenye makroni 50 peke yake.

**SPIKA:** Swali linalofuata kwa Wizara inayofuata ya Nishati na Madini naona Mheshimiwa Zitto Kabwe hayupo, Ahh, kuna majibu ya nyongeza ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana na fasaha ya Naibu Waziri ningependa kuongeza na kulitaarifu rasmi Bunge lako Tukufu kwamba ndani ya Serikali tunafanya mazungumzo pamoja na kuwahusisha wadau mbalimbali na naamini wakati wa bajeti ya Wizara yetu tutakuwa tumefikia muafaka, dhamira ni kwamba tarehe 1 Januari, 2017 iwe mwisho wa matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini, lakini tutafika pahala ambapo uamuzi huo utakapofikia basi tutalitaarifu Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, kama nilivyosema Wizara inayofata, ni Mheshimiwa Zitto hayupo, nimemuona Mheshimiwa Keissy amesimama kwa niaba ya Mheshimiwa Zitto.

Na. 5

**Mradi wa Kuzalisha Umeme Malagarasi**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. KABWE Z. R. ZITTO)** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa kuzalisha umeme wa Malagarasi utaanza?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Nishati na Madini Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya tafiti za kimazingira kuonesha kuwa utekelezaji wa miradi wa kuzalisha umeme katika Mto Malagarasi katika maeneo ya Igamba Na. III ungekuwa na athari za kumazingira, Serikali itafute eneo lingine. Eneo la Igamba Na. III, lilipatikana na Mkandarasi Mshauri *ESBI* alianza kazi ya upembuzi yakinifu mwezi Juni, 2010 kupitia ufadhili wa Mfuko wa Changamoto za Milenia *(MCC I)*. Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali *(preliminary design)* ulikamilika mwaka 2012 na kubainika kuwa maporomoko ya sehemu hiyo yana uwezo wa kuzalisha MW 44.8 na Mkandarasi Mshauri alipewa kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na utekelezaji wa miradi kufanywa na Mfadhili mwingine.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa *TANESCO* inaendelea na taratibu za kumpatia Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina yaani *(detail design)* na kutengeneza nyaraka za zabuni *(tender document)* zitakazotumika kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kazi hiyo. Mradi huu unakusudiwa kutekelezwa kwa njia ya *EPC* (Uhandisi, Manunuzi pamoja na Ujenzi).

Mheshimiwa Spika, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri zitakamilika mwezi Juni, 2016, kazi ya usanifu wa kina pamoja na taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi itachukua miezi sita. Mkandarasi atakayepatikana ataanza kazi Februari, 2017 na utekelezaji wa mradi utachukua miaka mitatu, fedha zitakazotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa utekelezaji wa mradi huu ni shilingi bilioni tano.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimwia Spika, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya zake zinaingiza gharama kubwa sana katika Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kwa kutumia majenereta, zaidi ya bilioni 160 kwa mwezi, kwa nini Serikali pamoja na Wizara ya Nishati na Madini isifanye haraka mradi huu ili kuokoa pesa kwa Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Nishati na Madini Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa shughuli za ugawaji wa umeme katika Mji wa Kigoma ni gharama kubwa na gharama alizozitaja Mheshimiwa Keissy kwa kweli ni kidogo siyo shilingi milioni 160 isipokuwa ni shilingi milioni 600 kila siku za mafuta tunatumia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uzito huo huo, ndiyo maana Serikali imesema itaanza ujenzi wa mradi huo wa Malagarasi ndani ya miezi sita kuanzia sasa, kuanzia mwezi Februari mwakani shughuli za ujenzi kwa ajili ya kuwapatia umeme wa uhakika wananchi wa Kigoma zitaanza. Kama nilivyosema shughuli hizi zitachukua miaka mitatu hivyo mwaka 2020 shughuli za ugawaji wa umeme katika Mji wa Kigoma zitakamilika na umeme utakuwa ni wa uhakika ambao haukatiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Silinde swali fupi la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato mzima wa uzalishaji umeme katika Mto Malagarasi umetumia vilevile fedha za Mfuko wa Changamoto za Milenia *(MCC I)*. Ninataka nifahamu kwamba watu wa *MCC* wamekuwa wakipeleka fedha zao nyingi kwenye mradi wa umeme, na sasa hivi wamejitoa.

Je, sasa Serikali itupe *commitment* ya miradi yote ya umeme ambayo fedha zake zilikuwa za *MCC,* sasa Serikali itatumia vyanzo gani kuhakikisha kwamba miradi iliyopangwa inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali hilo isingekuwa vizuri likasubiri bajeti ya Nishati na Madini? Lakini Naibu Waziri kama unaweza ukajaribu haya tafadhali!

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba *MCC* wamejitoa kwenye mradi wa Awamu ya Pili, lakini kazi ya *MCC* iliyofanyika awamu ya kwanza ilifanyika vizuri, na pesa zote zilitumika. Sasa Serikali inafanyaje.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya mradi huu wa 2016/2017, nichukue mfano kwa Mto Malagarasi shilingi bilioni moja ilikuwa ni fedha za ndani, lakini dola za Marekani bilioni moja pamoja na zingine dola za Marekani bilioni tatu zitafadhiliwa na *World Bank* pamoja na Benki ya Dunia ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *MCC* kujitoa halijaharibika jambo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa.

Na. 6

**Mradi ya Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Liganga**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Wananchi wa Ludewa wamekuwa wakisikiliza mipango ya Serikali juu ya miradi mikubwa ya Makaa ya Mawe, Mchuchuma na Liganga ambapo kumekuwa na mipango mingi ambayo kwa sasa inaonekana kutekelezwa:-

(a) Je, ni lini wananchi walioachia ardhi yao kupisha miradi hiyo watalipwa fidia?

(b) Je, ni lini miradi hiyo inatarajiwa kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga inasimamiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji lakini inafanywa hivyo kwa kupita Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)*. Miradi hii inaendelezwa kwa pamoja kwa maana ya *(Intergrated Projects)* kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* lenye asilimia 20 ya hisa na Kampuni ya *Sichuan Hongda (Group) Company Limited* ya China yenye hisa asilimia 80 kupitia kampuni ya ubia *Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa leseni za uchimbaji mkubwa *SML* namba 533/2014 ya tarehe 09/10/2014 katika eneo la Liganga lenye ukubwa wa kilomita za mraba 30.41. Lakini *SML* ya pili namba 534/2014 ya tarehe 9/10/2014 katika eneo la Mchuchuma lenye ukubwa wa kilomita za mraba 25.46. Leseni hizi zilitolewa kwa kipindi cha miaka 25 na zitaisha muda wake tarehe 08/10/2039.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ilifanya uthamini wa mali za wananchi walioko ndani ya maeneo ya miradi ambao walitakiwa kupisha shughuli za utekelezaji wa miradi mwezi Agosti, 2015 na kuridhiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali mwezi Agosti, mwaka huo huo. Mpango wa kulipa fidia unatarajiwa kuanza mwezi Juni, mwaka huu chini ya usimamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi unatarajiwa kuanza Machi, 2017 na kukamilika mwezi Julai, 2020 na utafanywa hivyo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ngalawa, Mbunge wa Ludewa swali la nyongeza!

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado ulipaji wa fidia huu umeonekana kuwa ni kitendawili, kwa mara ya kwanza tuliambiwa kwamba fidia hizi zitalipwa tarehe 16 Februari, lakini sasa hivi Serikali inakuja na majibu mengine kwamba itaanza kulipa mwezi Juni. Sasa tunaomba kujua *specific date* ya fidia hiyo itakuwa ni lini?

Pili, kumekuwa na usumbufu mkubwa katika ulipaji wa hiyo fidia, je, kwa sababu muda utakuwa umeshapita fidia hii italipwa pamoja na fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli fidia ilianza kulipwa tangu mwezi Februari mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, lakini tutambue kwamba suala la ulipaji fidia ni suala endelevu, kadri tathmini inavyofanyika ndiyo fidia inavyoendelea kulipwa na ndiyo maana tunasema hata mwezi huu na mwezi ujao wataendelea kulipwa fidia. Suala kubwa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba shughuli za ujenzi wa mradi huu zitaanza mapema tu baada ya fidia kukamilika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kama wananchi watalipwa pia pamoja na nyongeza ya mapunjo ya awamu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, taratibu za fidia kwa waathirika hufanyika wakati tathmini inapofanyika, kwa hiyo malipo ya fidia hulipwa kulingana na viwango wakati tathimini inafanywa na siyo vinginevyo.

**SPIKA:** Tafadhali Mheshimiwa Upendo swali la nyongeza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa fidia Ludewa pia linafanana na sehemu ya Wilaya ya Geita ambapo wananchi wa mtaa wa Mgusu wanaishi katika eneo ambalo liko ndani ya *beacon* ya *Geita Gold Mine* na wananchi hawa wamekuwa wakiathirika na taka zenye sumu zinazomwagwa katika eneo lao.

Je, Serikali inaweka msukumo gani kwa *Geita Gold Mine* kuhakikisha kwamba inawalipa wananchi wa mtaa wa Mgusu fidia ili waweze kupisha eneo hilo na wasiathirike na taka katika hilo eneo la Geita? Asante.*(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa wananchi wa Mgusu wanaishi sehemu ya leseni ya utafiti wa *GGM,* lakini taratibu ya Sheria za Ardhi na Sheria za Madini zote hulingana. Kimsingi, mahali ambapo mgodi haulitumii eneo hilo wananchi wanaweza waka-*co-exist* na shughuli za mgodi, lakini mahali ambapo shughuli za mgodi zinafanyika, basi wananchi wanaoishi katika maeneo hayo hufanyiwa fidia na kupisha shughuli za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mgusu linalozungumzwa, Mgodi wa *GGM* haujaanza kulitumia. Kwa sasa hivi wananchi wanaishi Mgusu na kimsingi Mgusu imeshakuwa ni mjini na *GGM* sasa hivi haioni sababu ya kulichukua. Ila itakapofika wakati wa kulichukua eneo hilo, Mheshimiwa Mbunge atawasiliana na sisi na taratibu za fidia za wananchi wa Mgusi zitafanyika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza.

Na. 7

**Matatizo yaliyopo katika Kituo cha Polisi Maruhubi**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Maruhubi kinakabiliwa na matatizo mbalimbali kama vile ukosefu wa askari wa kutosha; kituo hakitoi huduma saa 24, lakini pia majengo yake ni machakavu sana kiasi kwamba hayana hadhi ya kuwa Kituo cha Polisi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka askari wa kutosha katika kituo hicho na kuhakikisha kuwa kituo kinatoa huduma zake kwa saa 24?

(b) Je, ni lini Serikali itayakarabati majengo ya kituo hicho ili yaendane na hadhi ya Kituo cha Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Maruhubi ni Kituo cha Daraja "C" ambacho taratibu za utoaji huduma kwa mujibu wa miongozo ya Jeshi la Polisi kitatoa huduma kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni na kuwa na askari wasiozidi 20.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itakifanyia ukarabati Kituo cha Maruhubi mara tu fedha zitakapopatikana.

**SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jibu la kisayansi. Swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Pondeza, Mbunge wa Chumbuni.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJAD:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Je, ni lini watapata fedha na ukarabati wa kituo hicho kwa sababu, eneo hili ni maarufu na lina matatizo sana ya huduma za kipolisi?

Kwa hiyo, kutoa nafasi kwa saa 12 tu haitoshelezi kwa sababu, kuna maeneo mengi ya uhalifu na historia inaonesha na ripoti zipo, lakini muda unakuwa ni mchache ambapo wananchi wakihitaji huduma za kipolisi wanashindwa kuzipata mpaka wazifuate sehemu za mbali na uhalifu unakuwa umeshatendeka. Je, Mheshimiwa Waziri haoni umuhimu kukipa kipaumbele kituo hiki kwa bajeti hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Pondeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maruhubi kinafungwa saa 12.00 jioni siyo kwa sababu ya ukosefu wa fedha, lakini kwa mujibu wa taratibu kulingana na *Police General Order (PGO)* Namba 287(9) inaeleza utaratibu wa vituo vya polisi vilivyo; kuna *class A, B* na *C*. Kwa hiyo, Kituo cha Maruhubi ni *Class C* ambacho kwa kawaida kinapaswa kifunguliwe saa 12.00 na kifungwe saa 12.00 jioni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, swali la nyongeza!

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika jibu la muuliza swali la msingi (b) alieleza kwamba yuko tayari kukarabati kituo cha polisi husika ambacho kimetajwa, lakini kituo cha

polisi cha Kengeja ni kibovu, chakavu, kinavuja na kuta zake zimeanza kudondoka na ni athari sana kwa polisi na kituo hicho mmerithi kutoka kwa wakoloni.

Je, hamuoni kwamba ni aibu na fedheha kwamba hamuwezi kukikarabati na inawezekana kikapelekea askari hawa kupoteza maisha? Hamuwezi kukarabati hata lile ambalo mmerithi kwa wakoloni!?

**SPIKA:** Nadhani hili siyo swali eeh! *(Kicheko)*

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakiri kabisa kwamba kituo cha Kengeja hali yake siyo nzuri, hata mimi niliwahi kufanya ziara pale, lakini siyo Kengeja tu, ni maeneo mengi ndani ya nchi yetu vituo vya polisi haviko vizuri sana. Kwa mfano, Mkoani ni zaidi! Nadhani Kituo cha Mkoani kina hali mbaya zaidi kuliko Kengeja.

Mheshimiwa Spika, kama alivyozungumza mwanzo Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba tuna mkakati wa kuvifanyia ukarabati vituo hivi na utaratibu huo utakuwa unaenda hatua kwa hatua kulingana na hali ya fedha itakavyoruhusu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Masoud uvute subira.

Na. 8

**Wakimbizi Kupewa Uraia**

**MHE. JOHN P. KADUTU (k.n.y. MHE. RICHARD P. MBOGO)** aliuliza:-

Mwaka 2009 Serikali iliwapa uraia wakimbizi toka Burundi walioingia nchini mwaka 1992 na wengine waliozaliana katika makambi ya wakimbizi ya Katumba, Mushamo na Ulyankulu:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapa wakimbizi waliosalia?

(b) Ili kuondoa hali ya sintofahamu katika Sheria ya Wakimbizi Na. 20 inayokataza mikusanyiko zaidi ya watu watano, je, ni lini Serikali itafuta hadhi ya makambi ya wakimbizi katika maeneo ya Katumba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, napenda kurekebisha swali hilo kwamba ni kweli mwaka 2009 Serikali iliwapa uraia wakimbizi toka Burundi walioingia nchini mwaka 1972 na siyo mwaka 1992. Pia hakuna Sheria ya Wakimbizi Na. 20 bali ipo Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998. Vilevile maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ni makazi ya wakimbizi na siyo makambi ya wakimbizi na hakuna mkimbizi aliyepo kambini aliyepewa uraia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Wakimbizi *(UNHCR)* ipo katika hatua za mwisho kufanya uhakiki kamili kwa

wakimbizi walengwa ili kutoa uraia kwa wanaostahili, kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi. Tunategemea hadi kufikia mwisho wa mwaka huu kazi hii itakuwa imekamilika ili taratibu za kutoa uraia kwa mujibu wa sheria ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 20 cha Sheria ya Wakimbizi Na. 9 ya mwaka 1998 kinahusu wakimbizi na hasa kililengwa kwa wakimbizi waliopo makambini katika makazi ya Katumba, Ulyankulu na Mishamo. Wengi wa wakazi wake sasa ni raia, sio wakimbizi. Kwa hiyo, kifungu hicho hakiwahusu kwa kuwa sasa wakazi wengi wa Katumba, Ulyankulu na Mishamo wameshapewa uraia. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI inaandaa utaratibu wa kufuta utengefu wa maeneo haya ili viwe vijiji vya kawaida kwa mujibu wa sheria.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa nimekuona!

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, je, Serikali iko tayari kuwahakikishia wananchi hawa ni lini wale ambao hawajaamua kubaki au kuondoka na kurudi Burundi? Kwa sababu siyo kweli kwamba watu wote wameshapata uraia; wako ambao hawajapata na hawajasema wanataka nini. Je, Serikali iko tayari kutoa tamko nini kifanyike?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Masauni!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna takribani wakimbizi 8,800 ambao hawajapatiwa uraia kati ya wale 162,000 na zaidi ya wale ambao walipatiwa uraia, lakini kulikuwa na sababu kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa sababu hizo ni kwamba wengine ni watoto wa wakimbizi ambao walizaliwa baada ya wazee wao kupata uraia, lakini wakati ambapo Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwa hajaidhinisha bado uraia. Wapo wengine ambao hawakupewa uraia; walinyimwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo hali zao za uhalifu na mambo mengine ambayo hayakuweza kukidhi vigezo na sifa za kupata uraia nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoweza kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwa wale ambao hawakupata uraia na wamekidhi vigezo na wameomba uraia, maombi yao yanashughulikiwa na yatakapokuwa yamekamilika watapewa uraia kwa wale ambao watakuwa wamekidhi vigezo.

**SPIKA:** Tunahamia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali litaulizwa na Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 9

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Musoma**

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma kuwa kwenye hadhi ya Kitaifa kama siyo Kimataifa ni wazo la siku nyingi.

(a) Je, ni lini uwanja huo utajengwa katika hadhi stahiki?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuwa na ndege zake ili Mbuga yetu ya Serengeti iweze kufikiwa na watalii kwa urahisi kutoka nje moja kwa moja kuliko kupokea watalii wanaofikia Kenya na kuishi Kenya?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha tunachopoteza kwa kutokuwa na ndege zetu wenyewe kuleta watalii hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Musoma ili kiendelee kutoa huduma kama ilivyokusudiwa. Katika mpango wa muda mrefu, Serikali inaendelea na maandalizi ya uboreshaji wa miundombinu ya kiwanja hicho ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kutumia fedha za mkopo toka Benki ya Dunia unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kazi hii ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unahusisha pia viwanja vya ndege vya Iringa, Njombe, Songea, Lindi, Kilwa Masoko, Tanga, Moshi, *Lake Manyara*, Singida na Kiwanja kipya katika Mkoa wa Simiyu ambapo viko katika hatua za mwisho na inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Spika, mpango mahususi wa Serikali kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania yaani *ATCL* katika siku za hivi karibuni ni kununua ndege mbili mpya zenye uwezo wa kubeba abiria 78 kila moja ili kuimarisha huduma ya usafiri wa ndege hapa nchini hiyo ikiwa ni pamoja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine ni kununua ndege nyingine mbili mpya zenye uwezo wa kubeba abiria 120 na 155 ambazo zinatarajiwa kufika hapa nchini mwanzoni mwa mwaka 2017 na 2018. Ndege hizo zikifika, zitaliwezesha Shirika la Ndege *ATCL* kurejesha safari zake za Afrika Kusini, Afrika ya Magharibi, Uarabuni pamoja na India. Idadi hii itafuatiwa na ununuzi wa ndege za ziada katika kuimarisha soko hilo. Hatua ya tatu ni kununua ndege ya masafa marefu kuelekea China, Mashariki ya Mbali, Jumuiya ya Ulaya na kadhalika. Hatua hii itakaribisha pia wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa spika, pia kuchukuliwa kwa hatua hizi kutawawezesha watalii wengi kufika Tanzania moja kwa moja kwa kutumia Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* wakiwemo watalii wa Mbuga ya Wanyama ya Serengeti.

(c) Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana suala hili kulitolea takwimu sahihi kwakuwa linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina zaidi. Aidha, faida ambazo nchi zenye Mashirika ya Ndege ya Taifa yenye nguvu huzipata ni kuimarika kwa uchumi wa Kimataifa pamoja na kuharakisha maendeleo zaidi. Watalii, wawekezaji na watu wa kawaida hupenda kuwa sehemu ya mataifa yenye usafiri wenye hakika wa ndege, hivyo kujengeka kwa uchumi wa nchi hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, nimekuona.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, natambua umuhimu wa upembuzi yakinifu na kwamba unaendelea katika ujenzi wa uwanja wa Musoma. Je, ni lini ujenzi wa uwanja wa Musoma utaanza rasmi?

Pili, nimesikitika sana kwa majibu namba (c), nanukuu: "Ni vigumu sana suala hili kulitolea takwimu sahihi kwa kuwa linahitaji kufanyiwa utafiti."
Mheshimiwa Spika, swali hili tangu nimelipeleka lina miezi mitatu. Je, jibu hili ndilo linaloendana na Hapa Kazi Tu? Ni lini swali hili litapatiwa majibu? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Merdad Kalemani!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuanza kwa uwanja wa ndege, kama nilivyosema ni mara tu baada ya ukamilifu wa upembuzi yakinifu ambao ulitarajiwa kuanza mwezi Februari, 2017.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na takwimu za kina, ni kweli kabisa ili kupata ulinganifu wa hasara unazopata ndani na nje; na unapofanya takwimu za kisayansi, ni lazima uangalie mapato unayopata ndani na mapato unayopata ambayo unayakosa kwa kukosa ndege ambayo inasafiri Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo unavyofanya ulinganisho siyo rahisi ukapata takwimu leo wakati unatakiwa ulinganishe na mataifa mengine pia yanapataje faida kwa matumizi ya ndege za aina hiyo hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tumalizie swali la mwisho kwa siku ya leo. Swali la mwisho ni la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini. Kwa niaba yake, nimeambiwa Mheshimiwa Kunti yuko tayari.

Na. 10

**Ulipaji wa Ushuru wa Huduma za Mitandao ya Simu**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA (K.n.y. MHE. PAULINE P. GEKUL)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la ulipaji wa ushuru wa huduma ambao ni asilimia 0.3 unaotozwa kutoka mitandao ya simu ambao kwa sasa Halmashauri zimeshindwa kukusanya ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa ushuru wa huduma za mawasiliano ambao ni asilimia 0.3 limekuwa ni tatizo kwa pande zote mbili yaani Halmashauri ambazo ndiyo zinakusanya kwa upande mmoja na kampuni za mawasiliano ambazo anakabiliwa na ugumu wa kuzilipa kwa upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, suala hili limejadiliwa na wadau kwa kuongozwa na Wizara yenye dhamana na Mawasiliano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMESEMI), hivi sasa inafanyia marekebisho Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 ili kuwezesha kukusanya ushuru wa huduma wa mawasiliano pamoja na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, hatua hii litasaidia sana kupatia ufumbuzi tatizo lililoelezwa na Mheshimiwa Mbunge kwa mapato kukusanywa sehemu moja na Halmashauri zote kupata mapato stahiki. Rasimu ya Sheria hiyo ikikamilika inatarajiwa kujadiliwa katika kikao cha wadau hivi karibuni.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Kunti!

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri, ni masuala yale yale kwamba tupo kwenye mchakato. Naomba kupata majibu katika maswali yangu mawili.

(a) Ni lini sasa TAMISEMI itakamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria hiyo ili Halmashauri zetu ziweze kujipatia mapato yake stahiki?

(b) Ni lini kikao hicho cha wadau kitakwenda kufanyika ili tuweze kuokoa mapato mengi yanayopotea katika sekta hii? Asante.

**SPIKA:** Namuona Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, majibu tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kumekuwa na kero kwa Waheshimiwa Wabunge wote katika Majimbo yote kwa sababu minara imeenea maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, kila mtu katika Jimbo lake ana mnara na kila mtu anatarajia kukusanya kodi. Lengo ni kuhakikisha Halmashauri zinapata mapato, ndiyo maana ofisi yetu imeona, kwa sababu suala hili linagusa Halmashauri zote, lazima tuwe na mfumo ambao utakuwa muafaka kuhakikisha kwamba fedha zinakusanywa hali kadhalika Halmashauri zinapata fursa ya kukusanya hayo mapato vizuri na ndiyo maana mchakato huo umeshaenda.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sana kikao cha wadau kimeshakamilika, na jukumu linalofanyika ni kwamba *paper* itaondoka katika Baraza za Mawaziri, itajadiliwa na itakuja huko. Hata hivyo, tumeenda mbali katika marekebisho ya sheria hii, tunaenda kuangalia suala zima la *crop cess*, watu wanajua ushuru wa mazao umekuwa ni changamoto kubwa sana.

Kwa hiyo, sheria hii inakutanisha mambo mengi ili mradi Sheria ya Fedha Sura Namba 290 itakapokuja hapa Bungeni, basi iweze kukidhi mahitaji ya Waheshimiwa Wabunge wote katika Halmashauri zao, fedha ziweze kukusanywa na wananchi wapate huduma bora. Asante.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri pia nawashukuruni sana, kwa siku ya leo ya mwanzo tumeanza vizuri. Sasa niende kwenye matangazo yaliyoko mezani kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba kumtambua mgeni rasmi wa Mheshimiwa Lucy Owenya ambaye ni mume wake Dkt. Owenya. Ahsante sana na karibu sana. Pia hajaja pekee, amekuja na wageni wengine 36. Wageni wa Mheshimiwa Owenya naomba msimame! Karibuni sana.

Mheshimiwa Lucy Owenya ameshajiunga na sisi hapa, endeleeni kumwombea afanye kazi nzuri. Asanteni sana. *(Makofi)*

Wako wageni 43 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, pale walipo wasimame! Wageni 43 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, karibuni sana. Wajomba zangu na shangazi zangu kutoka Iringa huko, Mheshimiwa Ritta Kabati anafanya kazi nzuri, tuendelee kumwombea dua. Asanteni sana. *(Makofi)*

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka; hapa ni funga kazi, maana yeye ameleta wageni 50! Wageni wa Semuguruka wasimame! Asanteni sana, naomba mkae. Tuendelee kumwombea Mheshimiwa Oliver naye afanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Leo tumeletewa mfano mzuri sana na Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum kwa kuleta wageni na sisi tulioko humu Bungeni tukumbuke kuleta wageni wetu kutembelea Bunge hili na kututembelea. *(Kicheko)*

Kuna tangazo la utawala, wanasema wanapenda kuwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa kuna Kampuni ya kuuza samani inaitwa *Jaffery Industries Saini Limited,* watakuwepo kwenye viwanja vya Bunge hapa Dodoma kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 16 Aprili kwa ajili ya maonesho ya huduma zitolewazo na kampuni yao. Hivyo Waheshimiwa wote mnaalikwa kwenda kujifunza pamoja na kuangalia aina ya samani na huduma zitolewazo na Kampuni hiyo.

Tangazo lingine linalotolewa na Ofisi pia, linatangaza kwa Waheshimiwa Wabunge wa Makanisa ya Kiprotestanti *(CCT),* mnaombwa kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne tarehe 19 Aprili, saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge wanasisitizwa kuhudhuria ili kuweza kupanga mikakati ya kupata uongozi wa Makanisa hayo ya Protestanti *(CCT)* kwa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo la Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho mazoezi yanaanza rasmi kwenye uwanja wenu wa kawaida wa Jamhuri na kwamba mazoezi haya ni muhimu kwa afya zenu na maandalizi pia ya michezo ya kirafiki ambayo yatakuwepo kila *weekend* tutakapokuwa hapa Dodoma. Aidha, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla anawaomba niwatangazie viongozi wote na Wajumbe wa Kamati Tendaji ya timu ya *Bunge Sports Club* kuwa mkutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kipindi cha maswali kwisha na msikose kufika.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho, naomba niwatangazie ratiba ya siku ya leo, tarehe 19 Aprili, 2016 na ratiba hiyo itakuwa kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba kikao cha Bunge kitaahirishwa leo mara tu baada mimi kumaliza tangazo hili, lakini baada ya kipindi hiki cha maswali, Waheshimiwa Wabunge wote tutaenda kwenya Kamati za Vyama vya Siasa, kwenye *Caucus* zetu mbalimbali. Sijapata taarifa kwamba UKAWA wanafanyia wapi *Caucus* yao.

**MBUNGE FULANI:** *(Aliongea nje ya microphone).*

**SPIKA:** Wapi? Basi, mtaambiana wenyewe asubuhi hii mara baada ya hapa kama kuna kikao au hakuna, lakini CCM wataenda CCM Makao Makuu kuanzia saa 6.00. UKAWA

wataambiana wenyewe. Saa 11.00 jioni kutakuwa na *briefing* kwa Wabunge wote itakayofanyika hapa hapa katika Ukumbi wa Bunge. Naomba sana muwahi hiyo saa 11.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, naomba sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.10 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 20 Aprili, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*